# NYENZO ZA MAKONGAMANO YA KIULIMWENGU TANZANIA

**Makongamano Ngazi ya Kanda:**
Machi – Aprili, 2022 – Tanzania

# NYENZO ZA MAKONGAMANO YA KIULIMWENGU TANZANIA

**Makongamano Ngazi ya Kanda:**
Machi – Aprili, 2022 – Tanzania

# Makongamano ya Kiulimwengu –Muhtasari wa Mada

**Mada ya 1—Muono wa Bahá'u'lláh kwa jamii ya wanadamu**

- Kusudi la jamii ya wanadamu/muumbo (yaani, dini ya kweli)
- Kuinua jumuiya hai ambazo zinachangia kwenye maendeleo ya kiroho na kimwili
- Ni nini Wabahá'í na wale wanaofanyakazi pamoja nao wanafanya
- Maswali kwa ajili ya majadiliano kwenye vikundi vidogo vidogo

**Mada ya 2—Umbali uliosafiriwa**

- Kuonyesha Filamu: Vidokezo vya Jitihada za Miaka Mia Moja
- Tafakarini juu ya jitihada za jumuiya ya Kibahá'í kwa kipindi cha miaka mia moja iliyopita
- Maswali kwa ajili ya majadiliano kwenye vikundi vidogo vidogo

**Mada ya 3—Ujengaji wa jumuiya hai**

- Sifa bainifu za jumuiya hai
- Umuhimu wa ibada na huduma, na uchangiaji kwa ajili ya usitawi wa kila mmoja
- Maswali kwa ajili ya majadiliano kwenye vikundi vidogo vidogo

**Mada ya 4—Jitihada za kielimu na taasisi ya mafunzo**

- Umuhimu Mkuu wa elimu
- Umuhimu wa taasisi katika kujenga vyote viwili; uwezo kwa ajili ya kutoa huduma na uwezeshaji wa kuchangia kwenye maendeleo ya jumuiya ya mahali na jamii
- Program za kielimu za taasisi
- Vijana: jukumu takatifu la taasisi
- Kuonyesha Filamu: Mfano wa Kuigwa
- Maswali kwa ajili ya majadiliano kwenye vikundi vidogo vidogo

**Mada ya 5—Uchangiaji kwenye mabadiliko ya kijamii**

- Kuwa wahusika wakuu wa maendeleo yetu wenyewe na yale ya jumuiya zetu
- Shughuli za kijamii
- Kushiriki katika mijadala ya kijamii
- Maswali kwa ajili ya majadiliano kwenye vikundi vidogo vidogo

**Maelekezo kwa waandaaji na waraghibishaji**

- Mazungumzo wakati wa majadiliano katika kundi kubwa na vikundi vidogo vidogo hujumuisha viwango tofauti tofauti vya ujihusishaji na hujitahidi kuchunguza dhana kwa "njia rahisi na ya kina, yakiingiza matumizi ya sanaa.

- Waandaaji na waraghibishaji wanahamasishwa kuchukua maudhui, yakiwemo uteuzi wa nukuu au marejeo, ili kwamba yaweze kufaa vyema zaidi hali na tajiriba za wale wanaoshiriki. Wanaweza kuchukua maudhui yaliyopo ikiwemo miongozo ya hivi karibuni kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, nyenzo za Kongamano la Vijana, matini za vijana chipukizi, na kozi za taasisi.
- Mazingira ya kongamano yanapaswa yawe ya kuvutia, ya shangwe na yaliyojawa hali ya kiroho.
- Maandalizi yanapaswa yafanywe kuhakikisha kwamba washiriki katika makongamano wanasaidiwa kwa pamoja, katika vikundi vya kifamilia, vikundi vya vijana au vikundi vilivyoundwa kulingana na maeneo kuelekea na hata nje ya kongamano.
- Wakati kusudi la vikao siyo lazima liwe kuandaa mipango kamili, mazungumzo lazima kiasili yaendelee hadi kufikia kufikiria njia za kivitendo zaidi kwa wale wanaoshiriki, na familia zao, kutoa mchango kwenye mchakato wa ujengaji jumuiya unaoendelea katika eneo lao.
- Itakuwa muhimu kusoma aya ya nne ya barua ya 30 Desemba 2021 kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Mabara ambayo huelezea jitihada za Wabahá'í na wale wanaofanyakazi pamoja nao kote duniani. Wakati wa 'Mada ya 1', kutakuwa na fursa ya kulichunguza jambo hili zaidi pamoja na washiriki. Ni sehemu tu ya aya hii iliyojumuishwa katika nyenzo; walakini, tafadhalini chukueni kutoka sehemu zingine za aya hii zinazoendana na mazingira yenu.

**Makongamano ya Kiulimwengu—Nyenzo**

**Mada ya 1—*Muono wa* Bahá'u'lláh kwa jamii ya wanadamu**

*Majadiliano katika kikundi kikubwa*

- ***Kusudi la mwanadamu/muumbo (yaani, dini ya kweli)***

  Bahá'u'lláh husema kwamba "kusudi ambalo kwalo watu wa umauti, kutoka katika hali ya kutokuwepo kabisa, wameweza kuingia katika milki ya uwepo, ni kwamba waweze kufanya kazi kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu na kuishi pamoja kwa mapatano na maelewano." Yeye Amefunua mafundisho ambayo hulifanya hili liwezekane.[1]

  Kujenga jamii ambayo kwa kutambua hushughulikia kusudi hili la pamoja siyo kazi ya kizazi hiki pekee, bali ya vizazi vingi vijavyo, na wafuasi wa Bahá'u'lláh huwakaribisha wote ambao hujishughulisha pamoja nao katika jitihada hii.[2]

- **Kuinua jumuiya hai ambazo zinachangia kwenye maendeleo ya kiroho na kimwili**

[1] *Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara*

[2] *kama hapo juu*

Humaanisha kujifunza jinsi ya kuibua jumuiya zilizoshamiri, zenye mtazamo wa nje; humaanisha jumuiya hizo kujifunza jinsi ya kuleta maendeleo ya kiroho na kimwili; humaanisha kujifunza jinsi ya kuchangia katika midahalo ambayo huathiri muelekeo wa maendeleo hayo.[3]

Muono wa mabadiliko ya mtu binafsi na ya pamoja yakitokea sanjari, juu ya msingi wa ujifunzaji wa Neno la Mungu na utambuzi wa uwezo wa kila mtu wa kuwa mhusika mkuu katika igizo la kina la kiroho, uliibua hisia ya juhudi za pamoja.[4]

'Abdu'l-Bahá hueleza kwamba kadiri sifa za ushirikiano na kusaidiana zinavyodhihirishwa na kundi la watu, "ndivyo zaidi jamii ya wanadamu itakavyosonga mbele katika maendeleo na kushamiri."[5]

- **Ni nini Wabahá'í na wale wanaofanyakazi pamoja nao wanafanya**

Roho zilizowashwa zikiinuliwa kupitia michakato ya Mpango….zimejidhatiti kwa ajili ya ushamiri wa wote, zikitambua kwamba ustawi wa watu binafsi umo kwenye usitawi wa jamii kwa ujumla….wao ni raia watiifu ambao huepuka kushiriki katika vyama vya siasa na kugombea vyeo vya kidunia. Badala yake, wanamakinikia kuzishinda tofauti, wakiweka pamoja mitazamo, na kukuza matumizi ya ushauriano katika kufanya maamuzi. Wanasisitiza sifa na mitazamo—kama vile uaminifu, ushirikiano na ustahimilivu—ambazo ni zana kwa ajili ya ujengaji wa utaratibu usioyumba wa kijamii. Wanatetea urazini na sayansi kama muhimu kwa ajili ya maendeleo ya jamii ya wanadamu.[6]

**…**pale idadi iongezekayo inaposaidia kujenga jumuiya yenye sura hii, nguvu ya Hoja kubadili hali ya maisha ya kijamii ya watu, hali kadhalika maisha yao ya ndani, hupata kuonekana zaidi.[7]

*3 Kama hapo juu*
*4 Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa Ridvan 2021 kwa Wabaha'i wa Ulimwengu*
*5 Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara*
*6 Kama hapo juu*
*7 Kama hapo juu*

- **Majadiliano katika vikundi vidogo vidogo (huchunguza maana za mada ikihusishwa na uhalisia wa eneo lenu)**

***Maswali:***

1. *Ni zipi sifa na matarajio ya mazingira na watu katika eneo lenu? Kwa mfano, sifa bainifu za mazingira, hali ya watu katika eneo kiidadi, vijana na wazazi, hali kadhalika uwezo na changamoto mnazoziona katika jumuiya yenu.*
2. *Je, ni jinsi gani muono huu wa Bahá'u'lláh kwa jamii ya wanadamu unavyokunjuka katika eneo leu? Ni mchango gani ambao kila mmoja wetu anaweza kuutoa kwa ajili ya "uboreshaji" wa jamii?*
3. *Ni maeneo gani ya mafundisho ya Bahá'u'lláh huitikia matarajio ya jumuiya yenu?*
4. *Jinsi gani ushirikiano na kusaidiana kunavyodhihirika baina ya watu binafsi, jumuiya, asasi na viongozi wa eneo? Toeni mifano ya ushirikiano kusaidiana baina ya watu binafsi, asasi na jumuiya katika eneo lenu.*
5. *Je, mnatumiaje ushauriano kama njia ya kufanya maamuzi ambayo yatasaidia kutokea kwa maendeleo ya kiroho na ya kimwili? Kuna nafasi gani za ushauriano na tafakari ya mara kwa mara katika eneo lenu?*
6. *Mnajifunzaje kuhusisha idadi iongezekayo katika mchakato wa ujengaji jumuiya zinazoshamiri kiroho na kimwili?*

**Mada ya 2—Umbali uliosafiriwa**

*Majadiliano katika kikundi kikubwa*

- Kuonyesha Filamu: *Vidokezo vya Jitihada za Miaka Mia Moja*
- Tafakarini juu ya jitihada za jumuiya ya Kibahá'í kwa kipindi cha miaka mia moja iliyopita

  Baada ya kuangalia filamu "Vidokezo vya Jitihada za Miaka Mia Moja", tumieni muda kutafakari juu ya ujumbe gani filamu inawasilisha na pia juu ya safari ambayo jumuiya ya Kibahá'í imesafiri, na maendeleo yaliyopatikana.

***Zingatia:*** *Watu binafsi wangeweza kubainiwa mapema ili kuwasilisha safari ambayo jumuiya ya Kibahá'í ya eneo katika hali shirikishi*

**Majadiliano katika vikundi vidogo vidogo (huchunguza maana za mada ikihusishwa na uhalisia wa eneo lenu)**

- **Tafakarini juu ya maendeleo ya jumuiya na jamii katika eneo lenu**

  Tafakarini juu ya umbali uliosafiriwa katika eneo lenu kwa miaka kadhaa katika muktadha wa jitihada za washiriki wa jumuiya ya Kibahá'í na marafiki zao. Hii inapaswa ijumuishe utambuzi wa hali ya sasa ya jumuiya na muono kwa miaka ijayo.

***Zingatia:*** *Watu tofauti tofauti sharti wahamasishwe kutoa tajiriba zao za namna gani jumuiya hali kadhalika michakato tofauti tofauti na shughuli zilizomo ndani yake zilivyopiga hatua. Familia na watu binafsi wanaoshiriki wanapaswa washauriane juu ya wapi wangependa kwenda kutoka hapa na kubainisha hatua muhimu zitakazofuata. Hapa matumizi ya sanaa yangeweza kuwa njia ya kuwahusisha washiriki wote.*

**Mada ya 3—Ujengaji jumuiya hai**

*Majadiliano katika kikundi kikubwa*

- ***Sifa bainifu za jumuiya hai***

...katika majiji na vijiji kote duniani Wabahá'í wanajishughulisha katika kuanzisha mtindo wa maisha ambamo idadi iongezekayo, bila kujali usuli, inaalikwa kushiriki…Mtindo huu wa maisha ya jumuiya unaibua jumuiya mpya hai na zenye kusudi ambamo uhusiano unaasisiwa kwenye umoja wa wanadamu, ushiriki wa wote, haki na huru dhidi ya chuki. Wote wanakaribishwa.[8]

[Kutokana na tajiriba za pamoja za ujmuiya za Kibahá'í kote ulimwenguni]

Ilitambulika kwamba baadhi ya shughuli za [ujengaji wa jumuiya] zilikuwa muitikio wa kawaida kwa mahitaji ya kiroho ya watu. Vikundi vya mafunzo, madarasa ya watoto, mikutano ya ibada, na baadaye vikundi vya vijana chipukizi zilijipambanua kuwa zenye umuhimu mkuu katika hili, na zilipofumwa kwa pamoja na shughuli zinazoendana, nguvu zilizozalishwa zingeibua mtindo hai wa maisha ya jumuiya.[9]

…moyo unaoinuka wa ushiriki wa wote katika kazi ya ujenzi wa jumuiya. Kiutendaji, hii humaanisha kuhamasisha idadi ya kutosha ya Wabahá'i wanaotumia muundo wa utendaji wa Mpango kiubunifu na kiakili kwenye uhalisia wa mazingira yao wenyewe popote waishipo kwenye klasta. Hujumuisha familia na waumini binafsi kufanya kazi kwa pamoja na kufanya uamuzi makini kujiona wenyewe kama sehemu ya kiini kipanukacho. Makundi kama hayo ya marafiki hujiingiza katika upanuzi wa duara la ushiriki katika shughuli zao kwa kujihusisha na mitandao ambayo wao ni sehemu yake—mitandao iliyoundwa kupitia mahali pa kazi au masomo, shule ya eneo hilo, au kiunganishi cha jumuiya cha aina nyingine—na kwa kuambatana na wengine ambao huinuka kuhudumu pamoja nao. Juhudi hizi zina manufaa makubwa.[10]

---

*[8] Kutoka barua ya 27 Desemba 2017 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi*
*[9] Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa Ridvan 2021 kwa Wabaha'i wa Ulimwengu*
*[10] Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara*

Ndani ya kila kituo chenye shughuli shadidi, mipangilio shirikishi huibuka miongoni mwa makundi ya familia, ambao huandaa shughuli za ujengaji jumuiya miongoni mwao wenyewe wakiwa na mtazamo wa kupanua ukumbatiaji wa shughuli kama hizo kwa kaya nyingi za karibu karibu; mtandao usio rasmi wa marafiki hutoa hamasa na usaidizi wa jitihada zinazoendelea.[11]

***Zingatia:*** *Watu binafsi wangebainiwa mapema kutoa tajiriba za mabadiliko ya watu binafsi, makundi, na sehemu za jumuiya ambazo zimetambuliwa kama matokeo ya mchakato wa ujengaji jumuiya. Hii itasaidia kukazia sifa bainifu za jumuiya hai kivitendo.*

- **Umuhimu wa ibada na huduma, na uchangiaji kwenye usitawi wa kila mmoja**

Mwenendo wa maisha ya kila siku katika maeneo kama haya unajiambatanisha na uibukaji wa utamaduni ambao ibada na huduma ni shughuli zinazothaminiwa zikijumuisha watu wengi kwa wakati mmoja. Mikusanyiko ya kusisimua ya jumuiya, iliyoandaliwa vyema—katika baadhi ya hali hadi kufikia kambi na matamasha—hutokea mara kwa mara zaidi, na muziki na nyimbo hutokeza kwa kiwango cha juu kwenye matukio kama haya. Kwa hakika sanaa kwa jumla, sehemu muhimu sana katika maendeleo ya jumuiya tangu mwanzoni, hujitokeza kipekee katika mazingira kama hayo kama njia muhimu ya kuchochea furaha, kuimarisha mafundo ya umoja, kusambaza maarifa na kuimarisha uelewa, na vile vile kuwafahamisha wale wa jamii pana zaidi kuhusu kanuni za Hoja.[12]

Ufuatiliaji wa kimpangilio wa Mpango…hupelekea kwenye kuibuka kwa mtindo wa jitihada ya pamoja unaojitofautisha siyo tu kwenye kujifunga kwa ajili ya huduma, lakini pia kwa mvuto wake kwenye ibada. …shuhudieni, mathalani, jinsi mikusanyiko ya ibada ilivyojifungamanisha katika kiini cha maisha ya jumuiya. Mikutano ya ibada ni fursa ambazo roho yoyote inaweza kushiriki, ikivuta pumzi ya manukato ya mbinguni, ikijipatia utamu wa sala, ikitafakari juu ya Neno la Uumbaji, ikisafirishwa kwenye mbawa za roho, na ikizungumza na Mmoja Apendwaye kabisa. Hisia ya urafiki na kusudi la pamoja hufanyizwa, hasa katika mazungumzo ya hali ya juu ya kiroho ambayo kiasili hutokea katika nyakati hizo na kupitia humo "mji wa moyo wa binadamu" unaweza kufunguliwa.[13]

….katika maeneo kama hayo, fikra za marafiki wanaofanya kazi kwenye ngazi ya umma huendelea kujihusisha na maendeleo na ustawi wa kila mmoja anayeishi katika viunga vyake. Asasi za Kibahá'í hujisikia kuwa makini zaidi katika wajibu wao kwa ajili ya elimu ya kiroho ya kizazi kizima cha watoto na vijana chipukizi, wengi wao ama hata kwa ujumla wao tayari wanaweza kuwa wanajihusisha katika shughuli za jumuiya.[14]

[11] *Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara*
[12] *Kama hapo juu*
[13] Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 29 Desemba 2015 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara
[14] *Kama hapo juu*

**Majadiliano katika vikundi vidogo vidogo (huchunguza maana za mada ikihusishwa na uhalisia wa eneo lenu)**

***Maswali:***

1. *Jinsi gani ninyi pamoja na wale mnaofanya nao kazi mnajifunza kupanua duara la ushiriki wa familia na watu binafsi katika shughuli za ujengaji jumuiya katika eneo lenu?*
2. *Jinsi gani mazungumzo juu ya mada za kiroho na utamaduni wa ziara za majumbani zinavyoimarishwa katika eneo lenu?*
3. *Kuna nafasi/matukio gani katika eneo lenu ambapo familia na watu binafsi huja pamoja kwa ajili ya ibada ya pamoja?*
4. *Jinsi gani* mikusanyiko ya "kusisimua" na "iliyoandaliwa vyema", yakiwemo makambi na matamasha yanavyochochea familia, watoto, vijana chipukizi au vijana kuwa sura ya eneo lenu?
5. *Jinsi gani utumiaji wa sanaa "huleta shangwe", kuimarisha "vifundo vya umoja", na kuchangia kwenye usambazaji wa maarifa?*
6. *Ni ipi baadhi ya mifano ya huduma au jitihada za pamoja katika eneo lenu ambazo zinachangia kwenye "usitawi wa kila mmoja", wakiwemo watoto, vijana chipukizi na vijana?*
7. *Jinsi gani utamaduni unaokua wa ibada na huduma unavyochangia kwenye mabadiliko ya maisha ya watu katika eneo lenu?*

**Mada ya 4—Jitihada za kielimu na taasisi ya mafunzo**

*Majadiliano katika kikundi kikubwa*

- **Umuhimu Mkuu wa Elimu**

1. Umuhimu wa elimu kwa dhana ya Kibahá'í ya mabadiliko wa kiroho na kijamii, hauwezi kukadirika. "Fikiria", Bahá'u'lláh anasema, "ufunuo wa mwangaza wa Jina la Mungu, Mwelimishaji.[15]

2. Mchukulie mtu kama mgodi uliosheheni vito vya thamani isiyo kadirika. Elimu pekee, ndiyo inayoweza kuusababisha ufichue hazina zake na kumwezesha mwanadamu kunufaika kutoka humo.[16]

3. Elimu takatifu ni ile ya Ufalme wa Mungu: inajumuisha upatikanaji wa ukamilifu mtakatifu, na hii ndiyo elimu ya kweli; kwani katika hali hii mtu huwa mlengwa wa baraka takatifu, mdhihirishaji wa maneno haya, "Hebu Tumuumbe mtu kwa sura Yetu, na Mfano Wetu." Hili ndilo lengo la ulimwengu wa jamii ya wanadamu.[17]

[15] Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara

[16] *Baha'u'llah, Nyaraka Zilizofunuliwa baada ya Kitab-i-Aqdas, pg. 162*

[17] *Abdu'l-Baha, Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa, ch.3.7*

4. Hitaji la msingi, la haraka mno ni uendelezaji wa elimu. Ni jambo lisilofikirika kwamba taifa lolote laweza kupata ufanisi na mafanikio isipokuwa kama jambo hili muhimu kabisa na la msingi limeshughulikiwa.[18]

- **Umuhimu wa mchakato wa taasisi katika kujenga yote mawili; uwezo wa kutoa huduma na kuwezesha kuchangia maendeleo ya jumuiya ya mahali na jamii.**

1. Umuhimu wa elimu katika kazi ya ujengaji jumuiya ni dhahiri, na katika uwanja wa shughuli za kijamii upatikanaji wa elimu unabakia kuwa mchango muhimu kabisa wa Wabahá'í katika sehemu kubwa ya ulimwengu.[19]
2. Tunaweza kufikiria kazi ya taasisi ya mafunzo, hivyo,kama utaratibu wa kudumisha elimu masafa kwa ajili ya kuchochea na kurahisisha maongezi haya endelevu [yanayohusu uendelezaji wa jamii kupitia mafundiisho ya Bahá'u'lláh]. Vipengele vikuu vya utaratibu huu hujumuisha "kikundi cha mafunzo", mkufunzi na seti ya nyenzo zilizobobea katika maandiko ya Kibahá'í, ambayo huelezea umaizi wa kiroho na ujuzi uliopatikana kupitia mchakato wa kutafsiri mafundiisho ya Bahá'u'lláh katika uhalisia [kwa ajili ya maendeleo ya jumuiya yao vile vile kwa ajili ya maendeleo ya jamii].[20]
3. Taasisi ya mafunzo haina kifani kama chombo cha kuifikishia kiutaratibu idadi isiyo na kikomo ya roho maji yaletayo uzima ya Ufunuo na maana isiyokwisha ya Neno la Mungu.[21]
4. ….ushiriki katika kozi za taasisi, unawaandaa marafiki wa Mungu kwa ajili ya kujihusisha kwa kina daima katika maisha ya jumuiya pana zaidi; unawajalia maarifa, umaizi na stadi ambazo zinawawezesha kuchangia siyo tu kwenye mchakato wa kuendeleza jumuiya yao wenyewe, bali kwa maendeleo ya jamii. Kwa kifupi, taasisi ni nyenzo yenye uwezo kwa ajili ya uachiliaji wa nguvu ya Imani ya ujengaji jamii.....[22]

***Zingatia:*** *Watu binafsi wanaweza kuabiniwa mapema ili waweze kueleza tajiriba zao na jinsi mchakato wa taasisi ulivyowapa ujuzi, stadi na umaizi kwa ili kuhudumia jumuiya. Wazazi wanaweza kubainiwa kutoa mifano ya mabadiliko ambayo wao wameyaona ndani mwa watoto wao, vijana chipukizi na familia kupitia kuhusishwa kwa programu zilizotolewa na taasisi ya mafunzo.*

[18] *'Abdu'l-Bahá, Siri ya Ustaarabu Mtakatifu, p. 127*
[19] *Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara*
[20] https://www.bahai.org/action/response-call-bahaullah/training-institute
[21] *Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara*
[22] *Kama hapo juu*

- **Programu za kielimu za taasisi**

1. [Nenzo za taasisi ya mafunzo] zinatoa tajiriba ya kielimu iliyofumwa pamoja na iliyoshikamana kutoka umri wa miaka mitano na zaidi hadi umri wa ujana chipukizi, na kuendelea hadi utu uzima, na hutumika kama mwenzi wa moja kwa moja wa mtindo wa shughuli zinazokunjuka kwenye ngazi za umma.[23]

2. Program za kielimu zinazotolewa na taasisi ya mafunzo zinajumuisha madarasa kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto, program ya uwezeshaji wa kiroho ya vijana chipukizi na vikundi vya mafunzo:

3. [Madarasa ya watoto huanzisha] utaratibu wa kudumu kwa ajili ya elimu ya mtoto ambayo itaenda sambamba na vyote viwili; wasiwasi unaoendelea kukua miongoni mwa wazazi kwa ajili ya vijana wao kukuza mifumo imara ya maadili na kuinua ongezeko la rasilimali watu ndani ya jumuiya.[24]

4. … program ya uwezeshaji wa kiroho ya vijana chipukizi [imejazwa] na makusudi yenye nguvu ya aina mbili, yote kwa ajili ya kukuza uwezo wao uliojificha [wa vijana chipukizi] na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii.[25]

5. Kikundi cha mafunzo ni kikundi kidogo ambacho hukutana mara kwa mara kwa ajili ya kujifunza nyenzo za kozi. Mtu yeyote mwenye umri kuanzia miaka kumi na tano, au zaidi, awe Mbahá'í ama la hukaribishwa kushiriki. Kikundi huletwa pamoja na mkufunzi anayehusika na taasasi ya mafunzo …. wale wote wanaoshiriki huonwa kama mawakala hai wa ujifunzaji wao wenyewe, na wakufunzi hujitahidi kujenga mazingira ambayo huhamasisha watu binafsi kuchukua umiliki kwa ajili ya mchakato wa kielimu ambamo wanahusika. Kikundi cha Mafunzo sharti pawe mahali ambapo huongoza kwenye uwezeshwaji wa kiroho na kimaadili wa watu binafsi.[26]

---

[23] *Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara*

[24] *Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 12 Desemba 2011 kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa*

[25] *Kama hapo juu*

[26] https://www.bahai.org/action/response-call-bahaullah/training-institute

- **Vijana: jukumu takatifu la taasisi**

1. Taasisi zinajua fika kuwa uachiliaji wa uwezo uliomo ndani ya vijana, ni jukumu lao takatifu; sasa tunawataka vijana wa Kibahá'í waone maendeleo ya taasisi ya siku zijazo katika mwangaza huo huo…. sharti watwae kila fursa—katika shule zao na vyuo vikuu, na katika sehemu zilizotengwa kwa ajili ya kazi, familia, au maingiliano ya kijamii—kuhamasisha roho zaidi na zaidi kunufaika na programu za taasisi. Baadhi ya vijana wataweza kutoa kipindi cha huduma—pengine hata kwa miaka inayofuatana—kwa utoaji wa elimu, hususan kwa wale ambao ni wadogo kuliko wao wenyewe; kwa wengi, kusaidia shughuli za taasisi itakuwa kipimo kilichopo daima cha maisha yao katika kipindi chote cha elimu yao na watakapokuwa wanatafuta riziki kutokana na taaluma zao katika ulimwengu huu; lakini isijekuwa kwa yeyote kitu kingine zaidi ya kujitoa kwa mapenzi yao.[27]

- **Kuonyesha Filamu:** ***Mfano wa Kuigwa***

*Majadiliano katika vikundi vidogo vidogo (huchunguza maana za mada ikihusishwa na uhalisia wa eneo lenu)*

***Maswali:***

1. *Je, ni jinsi gani kikundi cha wale wanaoshiriki katika kozi za taasisi kinaweza kupanuka ili kuinua uwezo wa kutoa huduma katika eneo lenu?*
2. *Nini kinahitajika (au vikwazo gani vinapaswa kuondolewa) katika eneo lenu ili kumwezesha kila mtu—kijana kwa mzee, wanaume kwa wanawake—kushiriki katika programu za elimu ya kiroho inayotolewa na taasisi ya mafunzo?*
3. *Mnauonaje mustakabali wa vijana katika eneo lenu? Ni changamoto gani zinazowakabili na ninyi pamoja na wale mnaofanya nao kazi mtawezaje kuwasaidia?*
4. *Mbali na programu za kielimu za taasisi ya mafunzo, vijana wanawezaje kutiwa moyo na kusaidiwa kuendelea na elimu yao ya juu (kwa mfano, kidato cha tano na sita, kozi za elimu ya juu zaidi)?*
5. *Ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa kuhakikisha kwamba utaratibu wa kielimu katika eneo lenu unakidhi ipasavyo mahitaji yote mawili; ya kiroho na kiakili ya jumuiya nzima tangu utotoni hadi utu uzima?*

---

[27] *Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara*

**Mada ya 5—Uchangiaji kwenye mabadiliko ya kijamii**

*Majadiliano ya kikundi kikubwa*

- **Kuwa wahusika wakuu wa ukuaji wetu wenyewe na ule wa jumuiya zetu.**

1. Ufunuo wa Bahá'u'lláh unahusika na mabadiliko yote mawili; maisha ya ndani ya jamii ya wanadamu na mazingira ya kijamii. Mchango unaotolewa na Wabahá'í hutofautishwa kwa mlengo wake wa ujengaji uwezo kwa ajili ya huduma; ni mbinu ambayo hutokana na imani katika uwezo wa kikundi cha watu kuwa wahusika wakuu wa maendeleo yao wenyewe.[28]
2. Ujengaji uwezo ndiyo shime ya mipango hii: inalenga kuwawezesha wahusika wakuu wa jitihada za pamoja kuimarisha misingi ya kiroho ya vijiji na ujirani, kushughulikia baadhi ya mahitaji yao ya kijamii na kiuchumi, na kuchangia kwenye mijadala inayoendelea katika jamii, wakati huo huo, yote yakidumisha mfungamano wa lazima wa mbinu na njia.[29]

***Zingatia:*** *Watu binafsi, wakiwemo vijana na wazazi, wangeweza kushiriki uwasilishaji wao juu ya jinsi ushiriki katika mchakato wa taasisi ulivyowawezesha kuwa wahusika wakuu wa maendeleo yao wenyewe na kuwapa zana kuhudumia jumuiya zao za mahali kupitia shughuli za kijamii na kuchangia kwenye mijadala katika jamii.*

- ***Shughuli za kijamii***

Shughuli za kijamii zikichukuliwa ipasavyo katika mapana yake, zinaweza kuanza kwa jitihada zisizo rasmi sana ama za muda mfupi zinazofanywa na watu binafsi au vikundi vidogo vidogo vya marafiki hadi kufikia programu za maendeleo ya kijamii na kiuchumi zenye viwango vikubwa vya utata na ubora zinavyotekelezwa na mashirika yenye uvuvio wa Kibahá'í. Bila kujali upana na ukubwa, jitihada zote za kijamii huhitaji utumiaji wa mafundisho na kanuni za Imani kwa ajili ya kuboresha badhi ya sura za maisha ya kijamii au kiuchumi ya watu, hata iwe kwa kiwango kidogo jinsi gani. Hivyo, jitihada kama hizo huainishwa na kusudi lake lililoelezwa la kukuza hali njema ya kimwili ya watu, kama nyongeza kwa usitawi wao wa kiroho.[30]

---

[28] *Kama hapo juu*
[29] *Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka barua ya 2 Machi 2013 kwa Wabaha'i wa Iran*
[30] *Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ujumbe wa Ridvan 2010 kwa Wabahai wa Ulimwengu*

- **Kushiriki katika mijadala ya kijamii**

Kinachohusiana kwa karibu na uwezo wa kushiriki katika shughuli za kijamii ni uwezo wa kuchangia katika mijadala ya kijamii. Moyoni, huu kimsingi ni uwezo tu wa kushiriki katika mazungumzo yanayohusu suala linalogusa maisha ya watu na kutoa mtazamo uliobobea katika kanuni na tajiriba za Kibahá'í. Ikiangaliwa kwa namna hii, ni ujuzi ambao Wabahaí wengi wana fursa ya kufanyia mazoezi takribani kila siku, mathalani katika masomo yao au kazi zao, na ambao hulelewa kwa kushiriki kwenye kozi za taasisi…. Fursa hutafutwa kushirikiana mtazamo wa Imani na viongozi wa jumuiya na watu walio katika mamlaka, na nafasi hutengenezwa ambapo wawakilishi wa makundi na maslahi mbalimbali wanaweza kusadiwa kufikia mtazamo wa pamoja kupitia ushauriano.[31]

- **Majadiliano katika vikundi vidogo vidogo (huchunguza maana za mada ikihusishwa na uhalisia wa eneo lenu)**

***Maswali***:

1. Tafakarini juu ya baadhi ya vikwazo vya kijamii na kiuchumi vinavyozuia maendeleo ya kiroho na kimwili katika eneo lenu. Ni kwa namna gani jitihada za ujengaji jumuiya zinavyosaidia kujenga ufahamu na kuondokana na vikwazo hivi?
2. Jinsi gani ninyi pamoja na wale mnaofanya nao kazi mnajifunza kuinua ufahamu kwa wenyeji juu ya sifa za kiroho na mitazamo ambavyo huhitajika kwa ajili ya uboreshaji wa jamii?
3. Je, ni ipi baadhi ya mifano ya shughuli za kijamii zinazojitokeza katika eneo leu?
4. Je, hali ya muingiliano na watu wenye mamlaka, viongozi wa maeneo na/au machifu ikoje na inachangiaje kwenye uendelezaji wa watu wa maeneo hayo?
5. Jinsi gani tunaweza kukuza uwezo kwa watu wengi zaidi na zaidi kuchangia kwenye shughuli na mijadala ya kijamii?
6. Ni zipi baadhi ya ishara za mabadiliko ya kijamii yanayotokea mingoni mwa watu katika eneo lenu?

---

*[31] Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara*

**Makongamano ya Kiulimwengu—Nukuu za nyongeza kwa ajili ya marejeleo**

**Mada ya 1—*Muono wa* Bahá'u'lláh kwa jamii ya wanadamu**

- **Kusudi la jamii ya wanadamu/muumbo (yaani dini ya kweli)**

Sasa kuhusu kanuni zetu za kijamii, yaani mafundisho ya Mtakatifu Bahá'u'lláh yalienea kwa mapana na marefu miaka hamsini iliyopita, nayo kwa kweli hujumuisha mafundisho mengine yote. Ni wazi na dhahiri kwamba bila mafundisho hayo, ukuaji na maendeleo ya jamii ya wanadamu kwa vyovyote isingewezekani. Kila jumuiya ulimwenguni inapata katika Mafundisho haya Matukufu utambuzi wa matarajio yake juu kabisa. Mafundisho haya ni mithili ya mti ambao huzaa matunda bora kabisa kuliko miti yote. Wanafalsafa, kwa mfano, hupata katika mafundisho haya ya mbinguni ufumbuzi kamili kabisa wa matatizo ya kijamii, na vile vile maelezo ya kweli na bora ya mambo yanayohusiana na masuali ya kifalsafa. Vivyo hivyo watu wa imani huuona uhalisia wa dini kuwa umefunuliwa kwa udhahiri katika mafundisho haya ya mbinguni, na kuthibitisha kwa uwazi na kwa uhakika kwamba ni tiba ya kweli kwa ajili ya maradhi na madhila ya jamii nzima ya wanadamu. Kama mafundisho haya bora yakisambazwa, wanadamu wangekombolewa kutokana na shida zote, kutokana na maradhi yote sugu na magonjwa. Vivyo hivyo, ndivyo zilivyo kanuni za Kibahá'í za uchumi, taswira ya matarajio ya juu kabisa ya tabaka zote zinazotafuta riziki na wachumi wa shule mbalimbali.

Kwa kifupi, sehemu zote na vikundi vinafanikisha matarajio yao katika mafundisho ya Bahá'u'lláh. Kwa kuwa mafundisho yanatangazwa makanisani, misikitini na katika sehemu zingine za kuabudia, kama iwe zile za wafuasi wa Buddha au wa Confucius, katika mikusanyiko ya kisiasa au miongoni mwa wayakinifu, na wote watashuhudia kuwa mafundisho huleta uhai mpya kwa jamii ya wanadamu na hujumuisha tiba ya papo hapo kwa ajili ya maradhi ya maisha ya kijamii. Hakuna awezaye kupata kosa katika mafundisho haya, la hasha, bali mara yatakapotangazwa, yote yatasifiwa sana, na wote watakiri hitaji lao muhimu kabisa, wakisema kwa mshangao, 'Kwa kweli huu ndiyo ukweli na hakuna kingine kando ya ukweli huu isipokuwa makosa dhahiri.'

*('Abdu'l-Bahá, Waraka kwa Dkt. Auguste Forel,The Bahá'í World, vol. XV, pp. 37–43)*

- **Ni nini Wabahá'í na wale wanaofanyakazi pamoja nao wanafanya**

Roho zilizowashwa zikiinuliwa kupitia michakato ya Mpango zinatafuta daima kupata uelewa wa kina wa mafundisho ya Bahá'u'lláh—"tiba yenye mamlaka ya kila ugonjwa"—na kuyatumia kwa mahitaji ya jamii yao. Zimejidhatiti kwa ajili ya ushamiri wa wote, zikitambua kwamba ustawi wa watu binafsi umo kwenye ustawi wa jamii kwa ujumla. Wao ni raia watiifu ambao huepuka kushiriki katika vyama vya siasa na kugombea vyeo vya kidunia. Badala yake, wanamakinikia kuzishinda tofauti, wakiweka pamoja mitazamo, na kukuza matumizi ya ushauriano katika kufanya maamuzi. Wanasisitiza sifa na mitazamo—kama vile uaminifu, ushirikiano na ustahimilivu—ambazo ni zana kwa ajili ya ujengaji wa utaratibu usioyumba wa kijamii. Wanatetea urazini na sayansi kama muhimu kwa ajili ya maendeleo ya jamii ya binadamu. Wanasimamia ustahimilivu na maelewano, na wakiweka juu kabisa katika fikra zao asili ya umoja wa jamii ya binadamu, wanamuona kila mmoja kama mdau muhimu wa kushirikiana naye, na wanafanya juhudi kuendeleza hisia ya kirafiki hata baina ya makundi ambayo kwa jadi yamekuwa na uhasama moja kwa jingine.

Wanatambua jinsi nguvu za uyakinifu na anasa za kidunia ziwazungukazo zinavyofanya kazi, na macho yao yapo wazi kabisa kwa udhalimu mwingi unaoendelea ulimwenguni, bado wana mtazamo sahihi juu ya nguvu ya ujengaji ya umoja na uwezo wa jamii ya binadamu kuwafikiria wengine kuliko nafsi. Wanaona nguvu iliyomo katika dini ya kweli katika kubadili mioyo na kushinda kutoaminiana, na hivyo, wakiwa na imani katika kile ambacho kimo katika siku za usoni, wanafanya jitihada kulea hali ambamo maendeleo yaweza kutokea.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Mabara)*

**Mada ya 3—Ujengaji jumuiya hai**

- **Sifa bainifu za jumuiya hai**

…katika majiji na vijiji kote duniani Wabahá'í wanajishughulisha katika kuanzisha mtindo wa maisha ambamo idadi iongezekayo, bila kujali usuli, inaalikwa kushiriki…Mtindo huu wa maisha unaojielezea mfungamano baina ya vipimo vya kimwili na kiroho vya maisha hujumuisha madarasa ya elimu ya kiroho ya watoto ambamo pia wanakuza utambuzi wa kina kwa ajili ya umoja wa kimsingi wa dini mbalimbali za ulimwengu; vikundi ambavyo huwasaidia vijana kupita katika hatua muhimu za maisha yao na kukabiliana na nguvu haribifu zinazowalenga hususan wao; vikundi vya mafunzo ambapo washiriki hutafakari juu ya asili ya kiroho ya uwepo na kujenga uwezo kwa ajili ya huduma kwa jumuiya na jamii; mikusanyiko kwa ajili ya ibada ya pamoja ambayo huimarisha tabia ya kiibada ya jumuiya; na, baada ya muda jitihada nyingi za maendeleo ya kijamii na kiuchumi huibuka. Mtindo huu wa maisha ya jumuiya unaibua jumuiya mpya zenye hai na dhamira ambamo uhusiano hujengwa juu ya umoja wa jamii ya wanadamu, ushiriki wa wote, haki, na kuwa huru dhidi ya ubaguzi. Wote wanakaribishwa. Kikundi, bila kujali hali wala usuli wa kidini, bila kujali kabila au mbari, na bila kujali jinsia au tabaka la kijamii—kuinuka na kuchangia maendeleo ya ustaarabu.

*(Kutoka barua ya tarehe 27 Desemba 2017 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

… jumuiya hai za mahali, zinazopambanuliwa kwa ustahimilivu na upendo na zinazoongozwa na hisia yenye nguvu ya dhamira na hiari ya pamoja, [ndio] mazingira ambamo vipawa vya wadau wote, wanaume, wanawake, vijana na watoto—vinakuzwa na nguvu zao huzidishwa katika utendaji uliounganika.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 26 Desemba 1995 kwa Kongamano la Bodi za Bara za Washauri)*

Jambo kuu kwa muundo wa utendaji unaokua katika klasta ni mabadiliko ya mtu binafsi na ya pamoja yanayosababishwa kupitia wakala wa Neno la Mungu….Kadiri mtu akuzavyo tabia ya kujifunza na tafakari ya undani sana juu ya Neno la Uumbaji, mchakato huu wa mabadiliko hujidhihirisha wenyewe katika uwezo wa kuelezea uelewa wake wa dhana za ndani sana na kuchunguza uhalisia wa kiroho katika mazungumzo ya maana….Kupitia mabadilishano ya aina hii, ufahamu wa nguvu za kiroho hukuzwa, uwili uonekanao hujiachia kwa umaizi usio tarajiwa, hisia ya umoja na wito wa pamoja huimarishwa, imani kwamba ulimwengu bora unaweza kuundwa huimarishwa, na kujifunga kwa utendaji hudhihirika.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa tarehe 29 Desemba 2015 kwa Kongamano la Bodi za Bara za Washauri)*

Kadiri Mpango mmoja ulivyourithi mwingine, na uhusikaji na kazi za ujenzi wa jumuiya ulivyokuwa na msingi mpana zaidi, maendeleo kwenye ngazi ya kitamaduni yalionekana zaidi. Mathalani, umuhimu wa uelimishaji wa kizazi kichanga zaidi, ulikubalika kwa mapana zaidi, kama ambavyo uwezo usio wa kawaida uliowakilishwa hasa na vijana chipukizi. Roho zikisaidiana na kuambatana kwa pamoja kwenye njia moja, daima ziliendelea kupanua duara la kuhimiliana, zikawa mtindo ambao nguvu zote zilielekezwa kwenye ujengaji wa uwezo kwa huduma iliyotarajiwa. Hata mwingiliano wa marafiki miongoni mwao wenyewe pamoja na wale wanaowazunguka ulipitia mabadiliko, kadiri utambuzi ulivyoinuliwa kuhusu nguvu ya maongezi yenye maana kuwasha na kuchochea hisia za kiroho. Na muhimu zaidi, jumuiya za Kibahá'í zilijitwalia mwelekeo uliozidi kutazama nje. Roho yoyote iliyokuwa pokevu kwa muono wa Imani ingeweza kuwa mshiriki hai—hata mwendelezaji na pokevu kwa muono wa Imani ingeweza kuwa mshiriki hai—hata mwendelezaji na mraghibishaji—wa shughuli ya kielimu, mikutano kwa ajili ya ibada na vipengele vingine vya kazi za ujenzi wa jumuiya; kutoka miongoni mwa roho kama hizo, wengi pia wangejitangaza imani yao kwa Bahá'u'lláh. Hivyo, wazo la mchakato wa uingiaji kwa makundi liliibuka ambalo kidogo lilitegemea juu ya nadharia na mawazo na zaidi juu ya tajiriba halisi ya jinsi idadi kubwa ya watu ingeweza kuipata Imani, kuifahamu, kujitambulisha na shabaha zake, kujiunga na shughuli na majadaliano yake, na mara nyingi kuipokea. Kwa kweli, kadiri mchakato wa taasisi ulivyoimarishwa katika eneo hadi eneo, idadi ya watu binafsi waliochukua sehemu ya kazi ya Mpango, ikiwafikia hata wale walioijua Imani hivi karibuni, ilikua kwa upesi mno. Lakini hii haikuwa inasukumwa tu na wasiwasi wa idadi. Muono wa mabadiliko ya mtu binafsi na ya pamoja yakitokea sanjari, juu ya msingi wa ujifunzaji wa Neno la Mungu na utambuzi wa uwezo wa kila mtu wa kuwa mhusika mkuu katika igizo la kina la kiroho, uliibua hisia ya juhudi za pamoja.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, Riḍván 2021 ujumbe kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

## Mada 4—Jitihada za kielimu na taasisi ya mafunzo

- ***Umuhimu mkuu wa elimu***

… Bahá'u'lláh aliichukulia elimu kama mojawapo ya mambo ya msingi sana ya ustaarabu wa kweli. Elimu hii, walakini, ili iweze kukidhi na kuwa yenye manufaa, kiasili sharti iwe yenye maarifa mengi na haipaswi kuzingatia tu upande wa kimwili na kiakili wa mtu bali pia vipengele vyake vya kiroho na kimaadili.

*(Kutoka barua ya 9 Julai 1931 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)*

- **Umuhimu wa mchakato wa taasisi katika kujenga yote mawili; uwezo wa kutoa huduma na kuwezesha kuchangia maendeleo ya jumuiya ya mahali na jamii.**

Mlolongo mkuu wa kozi umeandaliwa ili kumwandaa mtu binafsi, awe Mbahá'í ama la, kwenye njia inayoelezewa na mkusanyiko wa tajiriba ya jumuiya katika jitihada yake ya kufungua muono wa Bahá'u'lláh wa Utaratibu wa Ulimwengu mbele ya jamii ya wanadamu. Dhana yenyewe hasa ya njia, ni wonesho wa asili na kusudi la kozi, kwani njia hualika ushiriki, inaashiria peo mpya, inahitaji juhudi na mjongeo, inaruhusu hatua tofauti tofauti na nyendo za kasi mbalimbali, ina umbo na mipaka. Njia yaweza kujaribiwa na kujulikana, siyo tu na mtu mmoja au wawili bali korija juu ya korija; inamilikiwa na jumuiya. Kuitembea njia ni wazo linalojieleza sawia. Inahitaji hiari ya mtu binafsi na chaguo; inahitaji seti ya stadi na uwezo lakini pia inavuta baadhi ya sifa na mielekeo fulani fulani; inashurutisha mwendelezo wa kimantiki lakini inakubali, pale panapohitajika, njia zinazolandana za uchunguzi; mwanzoni inaweza kuonekana ni rahisi lakini inakuwa yenye changamoto zaidi kadiri inavyoendelea. Na kwa umuhimu, mtu huitembea njia akiambatana na wengine.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, barua ya 12 Desemba 2011 kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa)*

…..mchakato ambao hutaka kuinua uwezo ndani mwa idadi ya watu kujitwalia dhima ya maendeleo yake yenyewe ya kiroho, ya kijamii na ya kiakili. Shughuli ambazo husukuma mchakato huu, na ambayo kwamo marafiki waliopatikana karibuni hualikwa kujishughulisha – mikutano ambayo huimarisha silika ya ibada ya jumuiya; madarasa ambayo hulea mioyo myororo na akili za watoto; vikundi ambavyo huelekeza nguvu zinazoumuka za vijana chipukizi; vikundi vya mafunzo, vilivyo wazi kwa wote, ambayo huwawezesha watu wa asili mbali mbali kuendelea kwa uhusiano ulio sawa na kuchunguza utumiaji wa mafundisho kwa maisha yao binafsi na ya pamoja….

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ujumbe wa Riḍván 2010 kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

…..ufahamu wa maana za Ufunuo, kuhusiana na ukuaji wa mtu binafsi na maendeleo ya jamii pia, huongezeka mara nyingi wakati ambapo mafunzo na huduma huuanganishwa na hutekelezwa kwa wakati mmoja. Hapo, katika uwanja wa huduma, elimu hujaribiwa, maswali huibuka kutokana na mazoezi, na ngazi mpya za ufahamu hufikiwa. Katika mfumo wa elimu ya mbali ambao umeanzishwa hivi karibuni katika nchi baada ya nchi – mambo ya asili yake makuu ambayo hujumuisha kikundi cha mafunzo, mkufunzi na mtaala wa Taasisi ya Ruhi – Jumuiya ya Kibaha'i ya ulimwengu imejipatia uwezo kuwezesha maelfu, la mamilioni, kujifunza maandiko katika vikundi vidogo kwa madhumuni dhahiri ya kutafsiri mafundisho ya Kibaha'i katika uhalisia,….

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ujumbe wa Riḍván 2010 kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

- ***Programu za kielimu za taasisi***

Mahali ambapo mpango wa ukuaji umeanzishwa katika klasta ambayo haijafunguliwa hapo awali, tunaona jinsi mishtuko ya mwanzo wa shughuli iibukayo kutokana na upendo kwa ajili ya Baha'u'llah uliomo katika moyo wa muumini aliyejifunga. Licha ya ugumu wa mipango ambayo hatimaye sharti iingizwe kadiri jamii ikuavyo katika ukubwa, shughuli yote huanza kwa uzi wa kawaida wa upendo. Ni uzi muhimu ambao kutoka kwake umefumwa mtindo wa juhudi yenye subira na juhudi za pamoja, duru baada ya duru, kuwafahamisha watoto wadogo, vijana, na watu wazima mawazo ya kiroho, kukuza hisia kwa ajili ya ibada kupitia mikusanyiko kwa ajili ya sala na ibada; kuamsha mazungumzo ambayo huangazia ufahamu, kuanzisha idadi ziongezekazo daima juu ya ujifunzaji wa maisha wa Neno la Uumbaji na kutafsiriwa kwake katika vitendo; kukuza pamoja na wengine, uwezo kwa ajili ya huduma; na kusindikizana katika zoezi la yale mafunzo yaliyopatikana.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ujumbe wa Riḍván 2015 kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

***Madarasa ya watoto***

Hebu wasisahau umuhimu wa kushughulikia mahitaji ya watoto wa ulimwengu na kuwapa masomo ambayo hukuza vipawa vyao vya kiroho na kuweka misingi ya tabia bora na adilifu.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 20 Oktoba 2008 kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

Watoto ni hazina zenye thamani kubwa mno ambazo jumuiya yaweza kuwa nazo, kwani ndani mwao kuna ahadi na uthibitisho wa siku zijazo….Mazingira hayana budi kudumishwa ambamo watoto hujisikia kwamba wao ni sehemu ya jumuiya na hivyo kushiriki kusudi lake…

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ujumbe wa Riḍván 2000 kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

***Vikundi vya vijana chipukizi***

Hebu waje watambue umuhimu kamili wa jitihada zao kuwasaidia vijana wadogo kujijengea utambulisho madhubuti wa kimaadili katika miaka ya ujana wao wa mwanzoni na kuwawezesha kuchangia kwenye usitawi wa jumuiya zao.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 20 Oktoba 2008 kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

Wanawasaidia vijana chipukizi kuongoza kupitia hatua muhimu ya maisha yao na kuwa waliowezeshwa kuelekeza nguvu zao kwenye uendelezaji wa ustaarabu.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa Riḍván 2008 kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

Wakati mielekeo ya ulimwengu huonyesha sura ya wakati huu ya kikundi cha hirimu hii kama tatanishi, iliyopotea katika machungu ya mabadiliko ya kimsukosuko ya kimwili na kihisia, isiyoitika na iliyoteketezwa na nafsi, jumuiya ya Kibaha'i – katika lugha iitumiayo na njia iichukuazo – inasonga mbele kwa vyovyote vile katika upande mwingine, ikiona katika vijana chipukizi badala yake ubinadamu, hisia kali ya haki, hamu ya kujifunza juu ya ulimwengu na tamaa ya kuchangia kwa ujenzi wa ulimwengu bora zaidi. Simulizi hadi simulizi, ambamo vijana chipukizi katika nchi zote duniani huelezea fikra zao kama washiriki katika mpango huu, huthibitisha juu ya uhalali wa muono huu. Kuna kila dalili kwamba mpango huu hushughulisha akili yao inayotanuka katika uchunguzi wa uhalisi ambao huwasaidia wao kuchanganua nguvu za ujengaji na uangamizaji zinazofanya kazi katika jamii na kutambua ushawishi nguvu hizi ziufanyao kwenye fikra zao na vitendo, zikinoa ufahamu wao wa kiroho, zikizidisha uwezo wao wa kujieleza na zikiimarisha miundo ya kimaadili ambayo itawasaidia katika maisha yao yote. Katika umri ambao nguvu zichipuazo za kiakili, za kiroho na za kimwili hupatikana kwao, wao wanapewa zana zihitajiwazo kupinga nguvu ambazo zingewanyang'anya sura yao halisi kama viumbe bora na kufanya kazi kwa manufaa ya wote.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ujumbe wa Riḍván 2010 kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

…..na ueneaji katika uwezo wa program ambayo huingiza ndani mwa vijana chipukizi hisia ya dhamira ya kimaadili ya aina mbili, kukuza uwezo wao wa kiasili ambao haujadhihirika na kuchangia kwenye mbadiliko wa jamii….

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ujumbe wa Riḍván 2010 kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

*Vikundi vya Mafunzo*

Maelfu kwa maelfu, wakikumbatia anuwai ya familia nzima ya wanadamu, wanajishughulisha na ujifunzaji wa kiutaratibu wa Neno la Uumbaji katika mazingira ambayo wakati huo huo ni makinifu na yanayosisimua. Kadiri wanavyojitahidi kulitumia kupitia mchakato wa utendaji, tafakari na ushauriano, umaizi unaopatikana kwa namna hii, wanauona uwezo wao wa kuhudumia Hoja ukiinuka hadi kufikia viwango vipya.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ujumbe wa Riḍván 2008 kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

….vikundi vya mafunzo, vilivyo wazi kwa wote, ambayo huwawezesha watu wa asili mbali mbali kuendelea kwa uhusiano ulio sawa na kuchunguza utumiaji wa mafundisho kwa maisha yao binafsi na ya pamoja…

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ujumbe wa Riḍván 2010 kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

*[Mkufunzi lazima atengeneze]* mazingira rafiki kwa ajili ya uwezeshwaji wa kiroho wa watu binafsi, ambao watakuja kujiona wenyewe kama mawakala hai wa mfunzo yao, kama wahusika wakuu wa mabadiliko thabiti ya mtu binafsi na ya pamoja kutumia maarifa ili kuleta mabadiliko binafsi ya pamoja.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ujumbe wa Riḍván 2010 kwa Wabahá'í wa Ulimwengu)*

- ***Vijana: jukumu takatifu la taasisi***

Licha ya hali zao za kijamii, vijana hutarajia kupata ukuaji wa kiroho na wa kiakili na "kutoa mchango kwa ajili ya fanaka ya jamii ya wanadamu". Wana nguvu nyingi ajabu, na kuzielekeza ipasavyo ni jambo muhimu, kwani zisipoelekezwa ipasavyo au kupotoshwa na wengine, zinaweza kusababisha mateso makubwa kwa kijamii. Miongoni mwa vijana wa Ulimwengu wapo wale ambao ni hai kwa muono wa Bahá'u'lláh wa ulimwengu wenye usitawi wa kiroho na kimwili. Kujihusisha katika programu za taasisi ya mafunzo huwawezesha wajione kama wale wanaotembea njia ya huduma. Sambamba na njia hii wanaendeleza uwezo wao kutumia mafundisho ya Bahá'u'lláh katika maisha ya kijamii. Wanaelewa, kama 'Abdu'l-Bahá alivyosema, kwamba hakuna kitendo ulimwenguni ambacho ni "bora zaidi kuliko huduma kwa maslahi mema ya wote", kwamba "uadilifu wa hali ya juu kabisa" ni "kuinuka na kwa nguvu kujitoa kwa ajili ya kutoa huduma kwa umma".

Katika huduma isiyo na ubinafsi kwa jamii kuna uwezekano wa yote mawili; ukuaji wa mtu binafsi na uendelezaji wa uwezo wa kuchangia maendeleo ya kijamii. "Huduma kwa jamii ya wanadamu ni huduma kwa Mungu", 'Abdu'l-Bahá amesisitiza. Kwa wale ambao wameinuka kuhudumu, Yeye amesihi, "Acha upendo na mwangaza wa Ufalme unururike kupitia kwenu hadi wote watakaowatazama waweze kuangaziwa kwa mwako wake." Kupitia uelekezaji wa vipawa na uwezo wao kwa ajili ya uinuaji wa jamii, wao "wanakuwa chanzo cha utulivu wa ulimwengu wa muumbo". Kadiri waingizavyo moyo wa utoaji wa ukarimu katika shughuli zao za kila siku, na kutoa vitendo vya hiari kwa ajili ya usitawi wa wengine, wanavutia msaada na mathibitisho ya Mungu.

Ni muhimu basi, kwamba, idadi iongezekayo daima ya wale ambao wamefikia upeo wa maisha yao "wajikaze kwa ajili ya maisha ya huduma" kwa jamii ….

*(Makongamano ya Vijana, Julai—Oktoba 2013, Nyenzo za Washiriki)*

**Mada ya 5—Uchangiaji kwenye mabadiliko ya kijamii**

- **Kuwa wahusika wakuu wa maendeleo yetu wenyewe na yale ya jumuiya zetu**

Nguvu za kiroho Walizoziachilia ulimwenguni ziliingiza uhai mpya katika kila eneo la jitihada, ambapo matokeo yake yapo dhahiri katika mabadiliko ambayo yametokea. Ustaarabu wa kimwili umepiga hatua pasipo kukadirika; mafanikio mapya ya kustaajabisha katika sayansi na teknolojia yamefikiwa; malango kuelekea maarifa yaliyorundikwa ya binadamu yamefunguliwa wazi. Na kanuni zilizowekwa na Baha'u'lláh kwa ajili ya uinuaji na maendeleo ya jamii na kwa ajili ya kukomesha mifumo ya kikandamizaji na utengwaji zimepokelewa kwa mapana. Hebu fikiria mafundisho Yake kwamba jamii ya binadamu ni wamoja, au kwamba wanawake wapo sawa na wanaume, au kwamba elimu lazima iwe kwa wote, au kwamba utafutaji razini wa ukweli lazima uzishinde nadharia za kinjozi na chuki. Katika mataifa yote, sehemu kubwa ya watu wa ulimwengu hivi sasa wanakubaliana na tunu hizi za kimsingi.

Hata hivyo, mabishano dhidi ya tunu hizi, ambazo awali ziliwekewa mipaka kwa watu wenye fikra makini, pia yanazuka tena katika jamii--kumbusho kwamba mawazo bora huhitaji nguvu ya msimamo wa kiroho ili kuyaunganisha. Kwa kuwa ni jambo moja kukitambua kitu fulani kikanuni; na ni lingine kabisa kukikumbatia kwa moyo wote wa mtu, na bado ni vigumu zaidi kuipa tena jamii mtindo kwa namna ambayo hutoa maana ya pamoja. Bado hii ni shabaha ya jumuiya zinazoibukia kote ulimwenguni ambayo ambayo huelekeana na mafundisho ya Baha'u'lláh.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa Oktoba 2019 kwa wote ambao wanakuja kutoa heshima kwa Mtangulizi wa Mapambazuko Mapya)*

- ***Shughuli za kijamii***

Kadiri ushadidi wa kazi ya ujengaji jumuiya uongezekavyo katika klasta, hapo marafiki bila kuepuka huwa na utambuzi zaidi wa vikwazo vya kijamii, kiuchumi au kitamaduni ambavyo vinazuia maendeleo ya kiroho na ya kimwili…..Katika kutafakari juu ya hali kama hizo inakuwa dhahiri kwamba, ndani ya klasta, upanuzi na uimarishaji, shughuli za kijamii, na uchangiaji katika mijadala inayoendelea ni vipengele vya jitihada moja, iliyounganishwa, yenye mtazamo wa nje inayotekelezwa kwenye ngazi ya umaa ya jamii. Jitihada zote hizi hufanyika kulingana na muundo wa pamoja wa kiutendaji, na hili juu ya mengine yote huleta mwambatano kwenye mtindo wa jumla wa shughuli.

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara)*

- **Majadiliano katika vikundi vidogo vidogo (huchunguza maana za mada ikihusishwa na uhalisia wa eneo lenu)**

  ***Maswali:***

1. Jinsi gani ninyi pamoja na wale mnaofanya nao kazi mnajifunza kuinua ufahamu kwa wenyeji juu ya sifa za kiroho na mitazamo ambavyo huhitajika kwa ajili ya uboreshaji wa jamii?
2. Je, ni ipi baadhi ya mifano ya shughuli za kijamii zinazojitokeza katika eneo leu?
3. Je, hali ya muingiliano na watu wenye mamlaka, viongozi wa maeneo na/au machifu ikoje na inachangiaje kwenye uendelezaji wa watu wa maeneo hayo?
4. Jinsi gani tunaweza kukuza uwezo kwa watu wengi zaidi na zaidi kuchangia kwenye shughuli na mijadala ya kijamii?
5. Ni zipi baadhi ya ishara za mabadiliko ya kijamii yanayotokea mingoni mwa watu katika eneo lenu?

**S.L.P. 585, Makongo Juu, Dar es Salaam, Tanzania.**
**Simu: +255-685 637 422**
**Barua Pepe: secretariat@bahai.or.tz., literature@bahai.or.tz**